# UZIMA

Sina ngumi, nina makumbatio. Nilikuwa nikipiga ngumi, kama mnavyojua, hapo awali, kwa namna fulani tu, nilitaka kufanya taaluma kutokana nayo. Kwa hivyo niliachana na huko kupiga ndondi muda mrefu uliopita, ila tu kwa ibilisi. Nilikuwa nikiwaza hapa asubuhi ya leo, nikila hivi . . . nikiangalia mezani, hivi tofauti, jinsi vilivyo . . . wanakula, wengine walikuwa na mayai, na wengine walikuwa na chapati maji, na soseji, na kadhalika, na hata hivyo sisi sote ni wanadamu. Inashangaza, sivyo, sote tungekuwa wanadamu, na tuwe na milo tofauti hivi?

2 Nafikiri hivyo ndivyo ilivyo tu katika mawazo yetu ya kidini. Mnaona? Tunafikiri sisi ni . . . Wengine hapa walisema walikuwa . . . walikuwa wa Foursquare, na wengine Assemblies, na wengine *hili*, *lile*, lakini hata hivyo, sisi sote ni Wakristo, mnaona, ni ninii tu . . . hivyo ndivyo ilivyo. Na huyo alikuwa ni Ndugu Courtner, niliyekuwa nikijaribu kumwazia, kutoka Foursquare, Ndugu Courtner. Bado yuko pamoja nao? [Mtu anasema, "Courtney."—Mh.] Courtney. Hakika ni mtu mzuri.

3 Kula chapati maji, nina hadithi ndogo juu ya hilo. Najua iko kando, ingawa inaweza isiende vizuri hivi sasa, lakini tunaelewa. Na—napenda kuvua samaki, nami napenda chapati maji. Na kwa hiyo, nilikuwa huko juu, huko juu kabisa New Hampshire, nimekuwa nikivua samaki wadogo wa maji safi, kwa namna fulani huko ndiko wanakoishi samaki wadogo wa kijito. Nami nilikuwa, nimejipakicha begi mgongoni mwangu yapata siku mbili, nami nilikuwa huko juu sana mlimani. Nami ni—ningewashika, mwajua, wakati nilipopata wawili au watatu wa kula, ninawaachilia wengine waende, napenda tu kuwashika. Kwa hiyo mimi . . . Kulikuwa na miti ya majini nyuma yangu, mikongoni ambayo ilikuwa ikinasa nzi wangu kila wakati, nilikuwa na hema dogo la mbwa, nami nikawazia, "Vema, sasa, kesho yake asubuhi nitaamka mapema, na kushuka kule, na kuipogoa miti hiyo." Kwa hiyo, loo, kulikuwa tu na samaki wadogo wa maji safi wakicheza tu chini ya hiyo, mwajua, ambapo maji yalikuwa yamewafagilia mbali, mwajua, huko nyuma matopeni, wazuri. Nami ningemkamata, nicheze naye, na kumrusha ndani upesi sana, mwajua, nisije nikamwua, na kisha kumfungulia tena. Kwa hiyo nikawaza . . . Loo, nilikuwa na wakati mzuri kweli.

4 Na kwa hiyo, nilishuka huko mapema, asubuhi hiyo, nikawaza, "Takriban hao hudhurungi wawili kwa ajili ya kiamsha kinywa watatosha tu pamoja na chapati maji kadhaa," mwajua, na kwa hiyo tayari nawapata wamechanganyana, kwa sababu siwezi kuwachanganya, mwajua, si—siwezi kuchemsha maji bila kuwaunguza, kwa hiyo si—sina budi tu kufanya hivyo.

Na kwa hiyo nikapanda kule, nami nikachukua ugwe wangu, nikaondoka karibu mapambazuko, nikafyeka vichaka hivyo, kisha nikawakamata samaki kadhaa, kisha nikawafungulia wengine, na kuwadhuru wachache kisha nikawarudisha.

5 Nikiwa njiani nikirudi ni. . .Enyi ndugu mnaowinda, mnajua jinsi ilivyo kwa maskini dubu mweusi kurandaranda wilayani. Kwa hiyo maskini dubu jike pale na watoto wawili walikuwa wameingia kwenye hema langu, kwa kweli walikuwa. . .waliichana vipande-vipande, nao hao hapo. Nikasikia kitu kikichakura, nikatazama pale, na huyu hapa maskini mama huyu ameketi pale pamoja na hawa watoto wawili, walikuwa ndio kwanza wachane kila kitu nilichokuwa nacho.

6 Nilijua sina budi kurudi, zaidi sana sio kile wanachokula, ni kile wanachoharibu. Na kwa hiyo, nilikuwa na kijishoka mkononi mwangu, nilikuwa na bastola kuukuu iliyokuwa imewekwa pale nyuma, lakini ilikuwa kwenye hema. Na hivyo, yeye. . .nao waninii. . .Loo, mama dubu kidogo atakushambulia, chochote kitafanya hivyo, mnajua, ikiwa unasumbua mahali walipo watoto wao. Nami kwa namna fulani nilikaa mbali, kisha nikaona mti ambapo ningeweza kuukimbilia upesi sana. Nami nisingetaka kumdhuru, na kuwaacha mayatima wawili msituni kwa vyovyote vile, mwajua. Kwa hivyo nilikuwa na kijishoka hiki mkononi mwangu. Kwa hiyo nikasema, "Ondoka hapo," naye akageuka, vema yeye, badala ya kunijia, alitoroka mbio, naye akaita watoto hawa, mwajua. Ndipo mmoja wa hao watoto akamkimbilia, maskini jamaa huyo mwingine alikuwa amenipa kisogo, ameketi tu *hivi*. Naam, nikawazia, "Kwa nini hukwenda, ewe jamaa mdogo?" Naye akaendelea kupiga kelele, akimwita mtoto huyo aje, asingekuja.

7 Vema, nikazunguka kando, kasema, "Huyu mtoto mdogo anavutiwa na nini, hata asiende kwa mama yake?" Ndipo akarudi nyuma hatua chache namna *hiyo*, nami nikautazama mti wangu, hivyo a—a—alikuwa anaelekea alipokuwa huyo mtoto, hata hivyo, kumfanya aje. Naye aliogopa kunikaribia, kisha akaogopa kumfikia huyo mtoto, ndipo akalia mara mbili ama tatu, kisha akarudi kwa mtoto wake mwingine. Basi maskini jamaa huyu alikuwa ameketi tu pale akifanya jambo fulani, nami nikashangaa jamani alikuwa anafanya nini. Kwa hiyo nikaendelea kuutazama mti wangu, nikizunguka kandokando.

8 Mnajua jamaa huyo mdogo alifanya nini? Nilikuwa na ndoo ya sukari ya rojorojo pale, ilikuwa, kwa ajili ya chapati maji zangu, maana napenda. . .Mimi ni. . .nilikuwa Mbaptisti, mwajua, nami sipendi kuzinyunyizia, ninapenda kuzibatiza kweli, kuzimwagilia, mwajua, vizuri. Nilikuwa na ndoo nzuri ya sukari ya rojorojo yapata ukubwa *huu*, naye maskini jamaa huyo alikuwa ameingia kwenye ndoo hii, sukari ya rojorojo, nanyi

mwajua jinsi wanavyopenda utamu, naye alikuwa ameondoa kifuniko, akaikumbatia mikononi mwake. Bila shaka, hakujua jinsi ya kuila, naye alikuwa akiingiza makucha yake ndani yake, akiilamba *hivyo*, mwajua, namna *hiyo*, akiilamba hiyo sukari ya rojorojo. Vema sasa, hiyo ilikuwa chapati maji ya mwisho pamoja na sukari ya rojorojo, niliona hivyo.

9 Kwa hiyo nikasema, "Toka hapo," wala asingenisikiliza, mwajua. Basi baada ya muda kidogo akageuka, na kuangalia, asingeweza kuyafungua macho yake, sukari ya rojorojo, mwajua, akiyavuta macho yake huku na huko namna *hiyo*, kitu cha kuvutia sana nilichowahi kuona, bila kamera, mnajua. Naye alikuwa sukari ya rojorojo kutoka juu ya kichwa chake hadi chini ya miguu yake. Nami nikasimama pale na kucheka mpaka mbavu zangu zikauma. Nikasema, "Hiyo ni kama tu mkutano mzuri wa Kipentekoste." Mnaona? Hiyo ni kweli. Kuingiza mkono wako katika ndoo ya asali hadi kwenye kiwiko chako, na kuanza tu kulamba, mwajua, wala hakuna hukumu wala hakuna woga.

10 Jambo la kushangaza, baada ya kumfukuza kutoka pale, aliingilia sukari yote ya rojorojo, akaimaliza kabla hajaondoka, ndipo akakimbilia pale alipokuwa mama yake na ndugu yake mdogo, nao wakaanza kumlamba. Hivyo ndivyo tunatarajia mkutano huu utaishia, hao wengine watajaribu kulamba baadhi ya hii asali, mwajua.

11 Hiyo ni njia fidhuli ya kujitambulisha, sivyo? Lakini mimi. . .hiyo ndiyo njia pekee niliyo nayo ya kulifanya, mnajua ninachomaanisha, nami nina hakika mnalielewa hivyo. Ni majaliwa makuu sana kuwa hapa pamoja nanyi ndugu asubuhi ya leo, na kujua ya kwamba—ya kwamba mnanifadhili katika hali ngumu. Mimi. . .Bila shaka, kama mjuavyo, kama Yeye akinifunulia jukwaani, Yeye. . .Mimi chini. . .Mnajua ninachomaanisha. Mnaona? Chini ya magumu mnafanya hivyo.

12 Mara nyingi, miongoni mwa mikutano, sijui ni kwa nini, lakini wakati mwingine watu wana maoni mabaya kuhusu kile ninachojaribu kufanya, ninajaribu kuvunja kizuizi kuwafanya watu wote walio Wakristo, ndugu katika Kristo, mnaona. Na wakati mwingine, kwa njia hiyo mimi huyakemea madhehebu, si kwamba ninapinga madhehebu, mnaona, hata kidogo. Jamani, sikujiunga na lolote, kwa sababu nilijisikia kama ningekaa kwenye pengo ningeweza kuwa na ushawishi mkubwa zaidi kuliko vile ningeweza kuwa nao nikielekeza ushawishi mdogo niwezao juu ya kundi fulani la watu. Nami naunga mkono sana mwenendo wa Kipentekoste. Nilikuwa mhudumu wa Baptisti ya Kimishenari, nilipoona jambo hili, hili lilikuwa *ndilo*. Na tangu wakati huo, nimekuwa na bidii sana kwa hao watu, ninawapenda.

13 Halafu basi, niko mbali sana na kuwa mwanahistoria, lakini

kutokana na kusoma historia kidogo, na kugundua kwamba kwa kawaida dhe—dhehebu ndilo—ndilo, linapokuwa lenye desturi sana hata haliwezi kumtambua mtu mwingine, Mungu huliweka tu kwenye rafu, halitumii tena.

14 Sasa, sitaki makundi yetu yawe hivyo, na—nafikiri dhehebu ni kitu kizuri sana, linadumisha udugu mzuri na safi, na, mwajua, li—linatimiza kusudi lake. Lakini sikuzote ninawataka wafike mahali ambapo mmoja angeweza kumkumbatia mwingine, na, mnajua ninachomaanisha, kushirikiana.

15 Kama vile mzee Ndugu Bosworth alivyoniambia, wakati mmoja, yule mzee mtauwa, mtakatifu, wengi wenu mlimfahamu, F. F. Bosworth, aliniambia, akasema, “Ndugu Branham, unaendelea kuzungumza juu ya ushirika. Unajua ni nini?”

Nikasema, “Nafikiri ninajua.”

16 Akasema, “Ni jamaa wawili katika meli moja.” Kwa hiyo niliwazia huo ulikuwa usemi mzuri sana, mnaona, jamaa wawili katika meli moja, basi kuna nafasi kwa ajili yetu sote.

17 Kama nilimwona ndugu yetu hapa, ndugu fulani, akishuka kwenye mto unaotiririka kwa kasi kwa mashua ndogo, ambapo nilijua mashua hiyo haitapenya kwenye viwimbi, mnaona, nami nikaanza kumpigia makelele, si kwamba ninamwonea huyo ndugu, ni upendo unaonifanya nifanye hivyo. Mnaona? Ni mashua aliyomo ndani yake, haitambeba. Mnaona?

18 Sasa, wakati madhehebu. . .Nafikiri kama dhehebu lingejiwekea taratibu halafu limalizie mafundisho yake kwa koma, badala ya nukta, “*Hili* ni *hili*, na *hili* ni *lile*, wala hukuna lingine.” Kama wakiweka tu koma, “Tunaamini *hili*, *pamoja* na kadiri Bwana anavyoweza kutuongezea.” Hapo ndipo Luther alipokosea, kuhesabiwa haki kwa imani, hamna lingine. Wesley alikosea kwa utakaso, kazi ya pili ya neema, ndipo akakataa kumpokea Roho Mtakatifu alipoingia. Ukimalizia kwa koma, sawa.

19 Kwa hiyo mnaona, Mungu ni mkuu sana, hema limetanda juu yetu sote. Nasi, huku tukila vyakula tofauti tofauti, kuvalia tofauti, kuonekana tofauti, sisi ni tofauti. Lakini Mungu ni Mungu wa aina mbalimbali, Yeye si Mungu. . . Yeye si Sears and Roebuck, Harmony House. Mnaona? Yeye. . .Mungu ni Mungu wa aina mbalimbali. Angalieni huku nje, milima mikubwa, milima midogo, miti ya kijani kibichi, majangwa, maua meupe, maua ya samawati, maua ya waridi, maua mekundu, watu wenye nywele nyekundu, wenye nywele nyeusi, na—na wenye mvi, halafu wasio nazo kabisa. Mnaona, Yeye ni Mungu wa vitu vya aina mbalimbali. Yeye. . .Ninaamini Yeye—Yeye anapenda hivyo, hivyo ndivyo alivyoyafanya. Nafikiri kwamba katika maisha yetu ya kimadhehebu kwamba Mungu anayo hivyo.

20 Mimi ni mtu wa kusini. Bwana mkubwa hapa anasema, taifa hili, wanayosema ni sawa. Nafikiri katika hali ya ubaguzi

wa kusini, baadhi yao waliniambia wakati mmoja, kasema, “Ndugu Branham, ukiwa mtu wa kusini, unawazia nini kuhusu ubaguzi?”

21 Nikasema, “Sio kwangu kusema. Bosi, serikali, ilisema, ‘Na iwe jinsi ilivyo, waruhusu waoane, na kadhalika.’” Nikasema, “Hiyo ni—hiyo ni juu yao, kama Mmarekani, na—nafuata sheria. Kwangu mimi, unapaswa kuiacha jinsi Mungu alivyoiweka, Yeye alimfanya mzungu, mtu mweusi, mtu wa kahawia. Yeye ni Mungu wa aina mbalimbali, waache wakae jinsi Mungu alivyowaumba,” hivyo ndivyo ninavyofikiria. Kama ningalikuwa mtu mweusi, ninge—ningetaka—ningetaka kukaa katika tabaka langu la watu; kama nilikuwa Mchina, manjano, na—na—nataka kubaki hivyo. Kwa kuwa mimi ni Muanglo-Sakson, mzungu, acha nioe miongoni mwa wazungu, niwafundishe watoto wangu vivyo hivyo, na kubaki tu aina ya ua na rangi ambayo Mungu alitufanya hapo mwanzo, hata hivyo, Yeye Ndiye aliyeifanya.

22 Kama mimi ni mfuasi wa Assemblies of God, ningekuwa Assemblies of God; kama nilikuwa wa Foursquare, ningekuwa Foursquare. Mnaona? Lakini sikuzote ningetaka kunyooshea kila mtu mikono yangu, mnaona, kuwakusanya wote pamoja. Mnaona? Ndivyo—ndivyo hivyo, shirikianeni. Hivyo ndivyo nimeeleweka vibaya.

23 Wakati mwingine. . .Nilikuwa na kanda iliyotolewa hapa si muda mrefu uliopita kuhusu. . .*Uzao Wa Nyoka*. Hiyo ilisababisha mzozo mkubwa. Poleni wavulana hao walizisambaza, hiyo ilikuwa katika ninii yangu—katika ninii yangu. . .hawako nami tena, lakini nasikitika walizisambaza hizo. Na hata hivyo, kama iliingia miongoni mwa makanisa. . . Najua kuwa hao wahudumu ni wachungaji, wanachunga kundi lao kwa ajili ya. . .na wasipofanya hivyo, wao si wachungaji wazuri. Hiyo ni kweli. Mnaona, ha—hawana budi kuliangalia kundi lao, na kwa hiyo, ambalo Roho Mtakatifu amewafanya waangalizi.

24 Kuna mambo mengi ambayo yamezungumzwa, tofauti, kila mtu ana wazo lake juu ya mambo, tuna haki kwa hilo, mnaona, kwa mawazo yetu. Lakini hiyo, ni—nisingeninii. . . hakika nisingeruhusu hizo zisambazwe. Lilikuwa wazo langu mwenyewe kuhusu kile nilichowaza katika Maandiko ya—ya, ya kwamba Hawa hakula matofaa ati yakasababisha dhambi. Na hilo. . .Kutokana na hilo, hata hivyo, lilionekana kusababisha maumivu, vurugu kati ya baadhi ya hao ndugu. La—laiti hazingesambazwa, kwa sababu, mnaona, mimi—mimi siko huku kujaribu kuwazuia ndugu zangu, niko huku, kujaribu kumsaidia ndugu yangu, ninafanya kazi kwa kusudi moja, nami nafikiri sote tunajaribu kufanya hivyo.

25 Na Assemblies, na—na Foursquare, na Umoja, na wowote

wale, mnaona, hao wote ni ndugu. Nasi, tunapaswa kuwa tukijaribu kupata fanaka moja, hilo ni Ufalme wa Mungu. Mnaona? Na nafsi nyingi kadri ninavyoweza kuwakusanya kwa wavu wangu kuwapeleka Huko juu, ninataka kuuweka pamoja na wako, na wako, na wengine wote. Huko ndiko tunakoenda, na huko ndiko tunakoshughulikia, ni huko Juu.

26 Nanyi mnatambua, miaka kumi na mitano hudumani pamoja na hao ndugu, hapana shaka mambo madogo yataibuka katika tofauti za mawazo. Sisi hawa hapa tumeketi hapa asubuhi ya leo kwa upatanifu kadiri watu wawezavyo kuwa, nadhani, lakini hebu tuketi hapa kidogo na tuanze kuzungumza, muda si muda mwajua, kungekuwa na ndugu fulani angesema jambo fulani, huyo mwingine—huyo mwingine anaweza kutokubaliana naye kidogo. Sasa, inahitaji watu halisi, Wakristo halisi, kustahimili hilo na bado wajisikie kama ndugu, mnaona. Unapaswa kuwa nalo moyoni mwako. Huwezi tu—huwezi—huwezi kudanganyia hilo. Ikiwa unasema ndivyo ulivyo, wala sivyo ulivyo, hiyo ndiyo iliyoshika. . . hiyo ndiyo—hiyo ndiyo inayozuia. Huna budi kuwa safi na wazi nayo, unaona. Na sisi—sisi tungekuwa tofauti. Kama vile, hebu chukua ninii fulani. . . kama ndugu alikuwa nje mahali fulani, na kuingia kati ya tabaka fulani la watu. . .

27 Ndugu mmoja alikuwa akinishuhudia asubuhi ya leo, aliitwa kwenye huduma akiwa mvulana mdogo, halafu basi akaanguka, alisema. Nami. . . Naye akasema, lakini basi akarudi na wito mwingi zaidi wa kuhubiri kuliko hapo awali. Mnaona jinsi ilivyokuwa, alipokuwa Mkristo, aliingia katika mazingira mabaya, mnaona, nayo mazingira hayo yakamshawishi. Mnaona? Nawe ukiendelea tu kushikilia mazingira ya aina hiyo, wewe. . . ya—yanakushawishi. Natumaini mnasoma katikati ya mistari, ninachosema, mnaona. Inakushawishi katika mazingira hayo, na muda si muda wajua, unakuwa sehemu ya mazingira hayo, unaingia ndani yake.

28 Na kama tu mtu mzuri safi, ambaye ni safi na mwadilifu, naye anaanza kushirikiana na kundi la watu wasio waadilifu, mnaona, unachukua roho ya kitu hicho. Kila kitu kinatawaliwa na roho. Mataifa yanatawaliwa na roho. Ninapoenda katika mataifa mbalimbali, nione jinsi wanavyofanya na kutenda, unaweza kuona ni roho ya taifa hilo.

29 Nilikuwa nikienda sokoni. . . Samahani, akina dada. Nilikuwa nikienda sokoni pamoja na mke wangu, hivi majuzi, na tulidhani ilikuwa ni kitu cha kigeni, tulimwona mama aliyevaa sketi. Karibu wote wako uchi, mwajua, wakiwa wemevalia kaptura hizo ndogondogo. Naye akasema—naye akasema. . . Nami nilijua wengi wao, pale, wanaimba katika kwaya, na mnajua, sawa tu, mnajua, m—mtu mashuhuri wa jijini.

30 Naye mke wangu ni mmojawapo wa hawa wasichana wa mtindo wa kale, mwajua, basi akasema, “Nashangaa kwa nini wanafanya hivyo.”

31 Nikasema, “Mpenzi, ni roho, unaona, inawaingia. Unaona? Ni roho, hao wanawake hawamaanishi. . .hawatambui wanalofanya. Unaona? Hawamaanishi hivyo, bali ni roho inayowaingia.” Na muda si muda mwajua, wanaanza kidogo tu, kisha zaidi kidogo, na ndivyo dhambi ilivyo (Ningesema nini?) janja, naam, janja, janja sana. Inanyemelea, ni nzuri sana, na ni janja sana, hivyo ndivyo inavyokuchukua.

32 Vema, nafikiri, mara nyingi, kwamba watu wazuri, wenye akili timanu huja kwenye dhe—dhehebu, nawe unapata, wakati mwingine, kwamba unapata mahali, mle ndani, ambapo kidogo ni. . .linaanza kutokea, “Sisi ndio kundi.” Mnaona? Na kwa kweli si udugu, kuna roho tu inayoingia miongoni mwao, mnaona, wala haimpi ndugu mwingine nafasi ya kutosha, mnaona. Na—nafikiri hiyo ni sawa, na ninaipata katika wote, nasi tunajua. . .Hilo ni sawa.

33 Kwa hiyo niko hapa, ndugu zangu, kutupa wavu wangu pamoja nanyi nyote, kufanya kila niwezalo kwa ajili ya—ya Mwokozi wetu mpendwa, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Si—si—sina. . .La, mimi si mhubiri, kusema tu mhubiri, kama ninyi watu mliosoma na kuitiwa hiyo, nina karama ndogo ambayo Mungu alinipa, na ni kama tu kuingizwa gia, siwezi kujiweka mwenyewe hapo.

34 Nilikutana na ndugu hapa, asubuhi ya leo, aitwaye Bacon, naamini ndiye, ama. . .Bacon, naamini ndiye, kule kwenye mghahawa, naam, kasema alikuwa hapa miaka mingi iliyopita nilipokuwa mkutanoni. Wakati huo lilikuwa ni tukio dogo tu la kuweka mikono yangu juu ya mtu fulani, kisha ningejua ilikuwa nini. Basi, mnakumbuka, niliwaambia ya kwamba Yeye aliniambia ya kwamba ingetokea kwamba ningejua siri ya moyo wao. Sasa, uangalie huu mkutano. Mnaona? Sasa, hiyo—hiyo ni kweli.

35 Lakini ni. . .Ni nini? Ambapo nimepungukiwa na kitu, Mungu, labda akijua kwamba ninawapenda watu, basi alinipa tu kitu kingine cha kutumikisha, mnaona. Wala sitaki. . .Na—nataka kulifanya kwa ajili ya mwili wote wa Kristo, kwa kila mtu, mnaona, nipate kujaribu kushawishi kila mtu niwezaye kumtumikia Bwana Yesu. Huenda nisieleweke na baadhi ya watu, lakini ninajaribu kuwatia moyo, wakae chini na kuliona Kimaandiko, kama halikuwa Maandiko, basi usiliamini. La, bwana.

36 Katika Agano la Kale walikuwa na njia ya kujua kama ilikuwa kweli au la. Kama nabii alitabiri, mwotaji akaota ndoto, walimpeleka mbele ya Urimu na Thumimu. Halafu basi. . .Hicho ni kifuko cha kifuani cha Haruni. Na—na

haidhuru ilisikika halisi jinsi gani, kama hizo nuru za kimbinguni hazikumulika pamoja na hiyo Urimu na Thumimu, hawakuiamini, mnaona, maana ilibidi iwe ya kimbinguni. Na kama Urimu na Thumimu haikuithibitisha, haidhuru hiyo ndoto ilisikika halisi jinsi gani, ama kile nabii alisema, ilikuwa ya uongo. Sasa, hiyo ilikuwa katika ukuhani wa Walawi. Nao ukuhani huo, umebatilishwa, hiyo Urimu na Thumimu imeondolewa, lakini Mungu angali ana Urimu na Thumimu, hiyo ni Neno Lake. Haijalishi jinsi mtu yeyote anavyosikika, anasikika kuwa sawa, au kama anasikika kuwa sawa kabisa ingekuwa programu, kwangu mimi, haina budi kumulika kwenye Urimu na Thumimu hiyo. Haina budi kuwa ni Neno hilo, la sivyo ni-. . .

37 Mnaona, ninii . . . naam, Mungu anaweza kufanya mambo, sasa tumekuwa na mambo ya kila namna yakiendelea, na, hapana shaka, watu watauwa, watu wema, lakini sisi . . . kama vitu tofauti, vya hisia, na damu, na mafuta, na kila kitu, hayo yanaweza yakawa sawa. Mnaona, Mungu anaweza kufanya hivyo, sisemi Yeye—Yeye hawezi kufanya, anaweza kufanya atakacho, Yeye ni Mungu, wala sina shughuli ya kumwambia la kufanya, Yeye hufanya atakacho. Lakini kwangu mimi, hebu liwe la Kimaandiko, basi ninajua ni kweli. Mnaona? Hebu liyamulike Maandiko hapo, basi hiyo—hiyo ni sawa, kwa maana ninajua Yeye atasimama nyuma ya *Hili*, sijui kuhusu lingine. Lakini najaribu kuliweka hivyo vizuri niwezavyo . . .

38 Wala si—siachi mikutano yangu kuwa mikubwa, ambapo ingewezekana nitenge ninii . . . kama vile baadhi ya ndugu zetu wa thamani, watu wazuri, kama vile Ndugu Oral Roberts . . . Wakati mimi na Oral tulipokutana kwa mara ya kwanza, alikuwa na hema dogo chakavu, nami nilikuwa upande mmoja wa—wa Jiji la Kansas, Kansas, naye alikuwa katika Jiji la Kansas, Missouri, ninayo picha yetu, tumesimama kule pamoja, akasema, "Unafikiri Mungu angenijibu kwa . . ." Vema, huyo hapo mtu, mwerevu, mwenye akili, mtu hodari wa Mungu, imani nzuri.

Nikasema, "Ndugu Roberts," mhudumu kijana tu, nikasema, "Mungu atajibu maombi ya mtu yeyote ambaye atakuwa mwaminifu." Huyu hapa anaenda.

39 Hivi majuzi . . . Ndugu wa thamani sana. Nilikuwa . . . alikuwa na mkutano, Wafanyabiashara, Tulsa, kisha nilikuwa na mkutano huko chini kwenye jumba la mikutano, ndipo Oral akaingia, mguu wake uliumia, naye akaniita kutoka jukwaani, nikaenda na kumwombea. Kasema, "Je, umeona ninii . . . jengo langu bado?"

Nikasema, "La, Ndugu Roberts, sijaliona."

Akasema, "Vema, mbona usiende kule ukaliangalie?"

40 Kwa hivyo kesho yake, nikaingia kisiri, huko, ili kwamba asiwepo, mwajua, sitaki kuninii . . . mtu mashuhuri . . . mtu kama huyo, najua wakati wake ni wa thamani. Kwa hiyo nikaenda, nikaketi nyumbani kwake, nisingeweza, nisingalitendewa mema zaidi kama ningekuwa nyumbani kwangu mwenyewe, Oral Roberts, jamaa mzuri sana.

41 Tommy Osborn, loo, jamani, kamwe hawavai kiatu cha ngozi vizuri zaidi. Ni hayo tu. Huyo . . . Yeye ni ninii tu . . . yeye ni mvulana wa thamani, nilikuwa nyumbani kwake, na loo, watu wazuri sana. Nao kama wote wanavyodai, ya kwamba nilikuwa wa kwanza hudumani, nao wakaiona, na hiyo ndiyo iliyowafanya waende.

42 Nikaenda huko basi, Ndugu Fisher, nilikuwa pamoja na kundi lake huko Afrika Kusini, alinionyesha jengo lote la Oral. Nikaangalia, mahali pakubwa mno, pa kupendeza. Endapo hujawahi kupaona, hakikisha utapaona. Loo, hujawahi kuona kitu kama hicho popote ulimwenguni.

43 Ndio kwanza niende kwa Ndugu Tommy Osborn na kuona mahali pake pazuri, mamia ya mitambo ya IBM imewekwa, ikifanya kazi hiyo, mikono ya binadamu haigusi hizo barua hata kidogo, [Ndugu Branham anadata vidole vyake mara kadhaa—Mh.] inajiendesha tu namna *hiyo*. Jamani! Pesa zikija kwa wingi mno, na kutupwa kwenye mkanda wa kuchukulia, na kushushwa chini. Niliwaza, “Loo, jamani!” Mnaona, hana budi kuwa nayo, yeye . . . Sikiliza, hiyo ni kazi kubwa.

44 Nami nikasimama pale nje, nikawaza, “Mungu, jinsi ninavyoshukuru, angalia hapa kwenye jengo hili hapa takriban dola milioni mbili na nusu, nadhani, unaona, mafanikio ya maskini mvulana mmoja wa Kipentekoste.” Yale Mungu anayoweza kufanya, mnaona, maskini Oakie mmoja kutoka shimoni kule chini, yale Mungu anayoweza kufanya, inaonyesha tu. Kisha nikamwona Tommy, Tommy Osborn.

45 Nikiwa nimesimama pale kwenye uga wa Oral, ningeninii . . . Kulikuwa na kundi la watu, mnajua jinsi wanavyokufanya, huku ukingojea huko nje, ndipo—ndipo polisi akanipitisha, na kunionyesha upande wa nyuma, jinsi ya kufikia mahali ningeweza kupata gari, naye Ndugu Fisher alikuwa azunguke, anichukue, kisha akaja akanichukua huko nyuma. Nami nilikuwa nimesimama huko nyuma nikitazama, mikono yangu nyuma yangu, nikitazama, jengo hilo kubwa, jinsi lilivyopendeza, na—na huku nikiangalia kioo mle ndani, mwajua, ile mikono iliyonyooshwa chini, ndipo nikawazia . . . Nami nikasema, “Vema, nina . . . ” Kitu fulani ndio kwanza kiniambie, “Vema, na wewe je?” Nikawaza, “Halafu hawa ndugu walisema kwamba huduma yangu ndogo ilisaidia kuwaweka hudumani.” Mnaona, kila mmoja wao aliketi na kuniambia hivyo.

46 Nami nikawazia, "Naam, nafikiri labda, kwa nini haikuninii. . .ambapo. . .Kama nilikuwa huko nje, kwa nini sikuwa na kitu kama hicho?" Mnaona? Nikawazia, "Hakika ningechukia wao kuja kwangu," taipreta moja iliyowekwa mwishoni mwa trela, huku nikimsihi mtu aje anisaidie kutuma barua. Nikawazia, "Vema, unaona, labda Mungu hangeweza kuniamini." Mnaona? "Labda kama ningeendelea hivyo, vema, nisingekuwa nilivyo mimi." Kisha nikawazia, "Lakini ninamshukuru Mungu sana kwamba angeweza kupata mtu ambaye Yeye angeweza kumwamini namna hiyo." Um-hum.

47 Nisingewataka mseme neno kuhusu. . .Silimaanishi hili vinginevyo, lakini nilipokuwa nimesimama pale nilianza kulia. Kisha nikawazia, "Vema, Baba alijua kwamba mimi, sina elimu. Hao wavulana, jinsi wanavyopendeza, wa thamani. . ." Niligeuka tu na kuanza kurudi nyuma, nikisubiri gari lije, nikasimama pale, nikalitazama jengo hilo kubwa, dhahiri sana kama nilivyopata kusikia sauti, ikasema, "Mimi ndimi Urithi wako." Sasa, hiyo ni—hiyo ni sawa. "Mimi ndimi Urithi wako."

48 Nikasema, "Asante, Bwana, basi kwa kile kidogo nilicho nacho, nitafanya niwezavyo kuweka sehemu uliyonipa kwa Ufalme wa Mungu."

49 Sasa, hivyo ndivyo nimejaribu kukaa, mdogo. Sina kitu, nasi tuna vitabu, lakini si vyangu, ni vya Ndugu Gordon Lindsay. Tunavinunua tu kwa asilimia arobaini tuwezavyo. . . Na inanilazimu kuwapa hao watu pesa, kurudi nyumbani, na kwa vile wanakuja Pwani ya Magharibi na vitabu hivi. Na vingi vyao vikaharibika, wanawapa watu, mtu yeyote anayevitaka, wasipokuwa na pesa zozote, mbona, wanaweza kuvichukua hata hivyo. Mnaona?

50 Kwa hiyo nilijaribu kukwepa pesa. Sikuwahi kuchukua sadaka maishani mwangu. Nami nikawazia, "Ningefanya nini ikiwa ningelazimika kufadhili kitu kikubwa?" Ni—nisingeweza kufanya hivyo. Ni ninii tu. . .Ni—nisingeweza kufanya hivyo. Hivyo tu. Kwa hiyo Mungu mkuu, asiye na kikomo alijua hivyo.

51 Kwa hiyo kile kidogo nilicho nacho ambacho amenipa, ninajaribu kukishiriki nanyi ndugu, mnaona, nyinyi ndio Kanisa, naomba sote tukae tu kitu kimoja, mnaona, na—na kukaa tu pamoja kama ndugu, na tushiriki tulicho nacho sisi kwa sisi. Mnaona? Kwa njia hiyo, tuko—tuko kwenye vita vikuu, nasi tu—tunapigana na dhambi, sio sisi kwa sisi, tu—tukipigana sisi kwa sisi, basi—basi Shetani anaweza kuketi kitako na kutuacha tu tupigane. Mnaona? Lakini hebu tuelekeze ninii yetu, kila kitu tulicho nacho kwenye Ufalme, na tuweke mabega yetu mmoja kwa-. . .na mwingine, tuanze kupanda juu, na tufanyie kazi huko, kwa sababu sidhani kama tuna muda mrefu zaidi, nafikiri tuko moja kwa moja mwishoni mwa barabara. Labda kwa sababu ninaanza kuzeeka ndiyo maana ninawazia

hilo, lakini mimi . . . la, sivyo ilivyo, kwa sababu niliwazia hayo sikuzote. Ni—ninaamini kwamba tuko mwishoni mwa barabara. Na tuombe, na kusaidia, na kuunga mkono.

52 Sasa, kuna Ndugu—Ndugu Roberts na hao wengine, wa—wa—wananinii . . . Mnaona, sasa, si—siwataki mwazie ya kwamba ninasema lolote dhidi ya Ndugu Roberts. Yeye ni mmoja wa watu walio bora sana niliowahi kukutana nao, Tommy Osborn, wengi, na Tommy Hicks, na hao ndugu ni ndugu wazuri, ninachojaribu kusema. Mnaona, pamoja na . . . Sasa, Ndugu Roberts, nafikiri, ana elimu ya chuo kikuu, yeye ni mwerevu. Naye ni . . . Naye Mungu amembariki sana mtu huyo hivi kwamba, anayo kila kitu karibu na yeye hapo tu kuangalia . . . Sisi sote watu, kama tukininii . . . Mungu ametugawia sehemu yetu, na kumgawia sehemu hiyo, lakini viungo vyote hufanya sehemu moja, mnaona, huenda kwenye Ufalme wa Mungu, mnaona, tunataka kujiweka pamoja.

53 Sasa, kama nikijaribu kujitenga na Ndugu Roberts, hilo lingekuwa ni kufanya jambo lile lile ambalo nimekuwa nikizungumzia, dhehebu moja likijitenga na lingine. Hebu tuwe kundi moja kubwa, mnaona, kundi moja tu kubwa.

54 Nikiwazungumzia Wafanyabiashara Wakristo, nimekuwa pamoja nao, kwa namna fulani wamekuwa oasisi kwangu. Na kwa sababu ya—ya kuwaacha wanifadhili, wafanyabiashara wa hayo makanisa watakuja, na, bila shaka, hiyo kwa namna fulani huifanya ionekane kana kwamba mchungaji karibu hana budi kufanya hivyo, mwajua, asije akaliaibisha kusanyiko. Lakini niliwaambia Wafanyabiashara, hapa si muda mrefu uliopita, nikasema, “Ndugu, mimi, kama yule ndugu alivyosema, ‘Si—sijawahi, kamwe sijawahi kuwa mnafiki vya kutosha kutokukemea chochote. Endapo ndivyo, ndivyo. Nikilisema, si kwa chuki yoyote, bali kwa upendo nalisema.’”

55 Kama mvulana wako mdogo, ama mtoto mdogo, alikuwa ameketi huko nje barabarani, nawe useme, “Kadogoo kipenzi, kama huingii ndani huenda utadhurika,” huo sio upendo; upendo wa kweli utatoka huko nje, na kumshika, na kumtikisa, na kumfanya akae mbali na barabara hiyo. Mnaona? Huo—huo ndio upendo wa kweli. Mnaona? Mnaona? Na hivyo—hivyo ndivyo ilivyo, ndugu. Simaanishi kwa lolote . . . Sasa, kumbukeni hilo. Mnaona? Sasa, usimdekeze Kadogoo, unaona, hatuna budi kumwambia Kadogoo, na kumfanya alainike. Mnaona?

56 Sasa, upendo wa udugu, ushirika wa pamoja, kufanya kazi pamoja, na kama vile tu kufanya mapatano na kadhalika, hivyo ndivyo tunavyojaribu kufanya katika Ufalme wa Mungu.

57 Sasa, katika wakati huu mkuu tunaoishi, ambapo tuko kwenye wakati wa mwisho, nafikiri . . . Sijui nina muda gani hapa. Kama dakika kumi na tano hivi? Tunashughulikia maisha, tunajitahidi sana kwa ajili ya maisha. Nasi ni . . . Na katika

mapambano haya ya maisha, tunaona kwamba sisi ni tofauti, lakini tuko sawa. Ninagundua kuwa kidole changu si sikio langu, na sikio langu si jicho langu, nami. . .lakini nagundua kwamba vimelazimika kufanya kazi pamoja ili kukamilisha kazi hiyo. Na hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya, mnaona. Inabidi tufanye kazi pamoja kuikamilisha kazi, ndiyo maana niko hapa, ni kujaribu kuikamilisha kazi. Sio kufanya kazi, siwezi kuifanya. Niko hapa kufanya kazi pamoja nanyi ndugu ili kuikamilisha kazi. Nafikiri uwezekano. . .Na inawezekana na huenda ikawa pia, kwamba hivi sasa jambo fulani linaweza kutokea, papa hapa, ambalo lingeeneza uamsho kupitia kila moja ya makanisa yenu, nanyi mnaona, lingeweza kufanya hivyo.

58 Sasa, jambo dogo linalonibidi kufanya, ninawashirikisha ninyi ndugu, nikiliweka juu ya madhabahu kuu ya dhahabu ya Mungu, pamoja na Dhabihu yetu na Misingi ya Pamoja, Yesu Kristo. Mnaona? Hapo tunafanya kazi. Nitafanya kazi na kila kitu ninachoweza, na chochote ambacho mimi. . .Mkiona kwamba ningeweza. . .mkiona ningeweza kufanya vizuri zaidi kidogo, iweni tu na uhuru wa kuniambia, mnaona, na hakika nitafanya hivyo. Nitafanya kila niwezalo kufanya moja kwa moja pamoja nanyi, kufanya yote niwezayo kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Na halafu, katika wakati wa mwisho basi, sote tutataka kumsikia akisema, "Ilifanywa vema, watumishi wangu wema na waaminifu."

59 Kumbukeni, mkutano huu hapa, utakuwa historia katika siku zingine tano. Mnaona? Halafu utakutana nasi tena siku moja. Kwa hivyo na tufanye kila tuwezalo kuufanikisha.

60 Ninajisikia tu kana kwamba ningependa kusema neno moja au mawili hapa ikiwa ni sawa kwa ninii kidogo tu. . .nataka—nataka kulinukuu Neno Lake mara moja, na labda tu, kidogo tu, kama somo na nitaangalia kwa makini sana. Hebu tuchukue Yohana Mtakatifu 5:24, mkitaka kulitafakari, ni mojawapo ya maandiko ninayopenda zaidi, konzi moja na dazani mbili za mayai, mnaona, 5:24.

> *Yeye alisikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenipeleka yuna uzima wa milele,*

61 Mnaona? *Uzima*. Ni neno la jinsi gani! *Uzima*. Tunafanya nini? Sisi ni. . .Huo ndio tunaojaribu kushikilia, uzima. Ndio tunaojaribu kutafuta, uzima. Ndicho kitu kikuu sana kilichopo, uzima.

62 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa nimeketi pamoja na katibu wangu kwenye kinjia kidogo kinachoelekea nyumbani, tukaokota kipande cha kale cha kisukuku, kilichokuwa humo ndani, akaniambia, kasema, "Kina umri gani hicho?"

Nikasema, "Loo, labda wanaelimuwendo, wanasema ingekuwa, au, waakiolojia wangesema kingekuwa karibu miaka milioni kadhaa."

Kasema, “Jinsi maisha ya mwanadamu yalivyo mafupi kwa hicho!”

Nikasema, “La, la, la.” Nikasema, “Wakati hicho hakipo tena, nitakuwa ningali hai.” Ninao Uzima wa Milele, unaona, na kwa hiyo . . .

63 Na tukitazama pande zote nafikiri, ndugu, kwamba tunaweza kuona kwamba kila mahali tunapoangalia ni uzima, uzima. Ukiangalia kupitia *hapa* unaweza kuona, labda, tuseme, ukiuona mchungwa, unadhihirisha uzima kwa njia yake wenyewe. Huu *hapa* mtende, unaonyesha uzima; huu *hapa* mti wa msonobari, unaonyesha uzima; lile *pale* ua, jekundu, linaonyesha uzima; lile la bluu lililosimama karibu nalo, linaonyesha uzima. Mnaona, madhehebu yetu? Mnaona? Mnaona, kila moja likionyesha uzima.

64 Tunaona ua dogo. Hebu tuchukue u—u—umuhimu wa ua dogo, linasimama pale, la kupendeza, linatumikia kusudi fulani, linalitumikia vyema. Ndipo wakati jalidi inapolipiga katika majira ya kupukutika mwakani, hiyo ni kusema, lililo changa ama lililokomaa, hufa. Hiyo ni mauti. Maskini petali zake zinapukutika, kisha mbegu ndogo nyeusi inaanguka kutoka kwake. Hebu tuone kama Mungu anavutiwa na kile tunachopambana nacho. Mbegu ndogo nyeusi inaanguka kutoka kwake, na baada ya kitambo kidogo basi, ni . . . ajabu kama inavyoonekana, Mungu anajali sana maisha hayo madogo mpaka anafanyiza maandamano ya mazishi kwa ajili yake. Ni, mvua ya masika inakuja, machozi makubwa mno yanadondoka kutoka angani, na kuizika mbegu hiyo ndogo. Sasa, hiyo ni kweli? Hakika ni kweli, yanaizika chini ya ardhi.

65 Moja kwa moja unakuja mgando wa kipupwe, unagandisha inchi kadhaa chini ya ardhi, maskini tunguu hilo linakauka, linaganda, linatoweka, petali zinaanguka, zimetoweka, jani limetoweka. Maskini ile mbegu ndogo inaganda, inapasuka, nyama inatoka, maskini uhai huo mdogo ambao Mungu aliumba. Je, umekwisha? La hasha. La, la.

66 Mnaona, mfumo wa jua unadhibiti uhai wa mimea, jua, j-u-a. Na mara tu jua hilo lenye joto linapoondoka kutoka nyuma ya dunia, na kurudi hapa karibu, kuna chembe ya uhai mahali fulani mle ndani ambayo hakuna mwanasayansi anayeweza kuipata, bali maskini ua hilo linaishi tena. Limetimiza kusudi lake, linaishi tena, kwa sababu ni uhai.

67 Vema, ikiwa Mungu alitengeneza njia kwa mfumo wa jua kuufufua tena uhai uliomtumikia Yeye, vipi kuhusu M-w-a-n-a anapokuja na Uzima wa Milele? Nasi tunao Uzima wa Milele, tutafufuka tena baadhi ya siku hizi. Hebu tutumikie tu kusudi letu vizuri, chochote tulicho, na tukitumikie. Mahali popote Mungu anapokuweka, tupatumikie, kwa maana M-w-a-n-a atachomoza moja ya siku hizi akiwa na uponyaji katika

mbawa Zake. Ninataka kutokea wakati huo, katika mng'aro na utukufu wa kufufuka Kwake. Ninataka kutembea nimeshikana mikono na kila mmoja wenu, Mbele Zake. Hadi wakati huo, kumbukeni, sisi ni lile jani dogo juu ya mti.

68 Ninapenda kuwinda. Nadhani mnaona uso wangu umelipuliwa. Sikuzote nilitaka Weatherby Magnum. Nanii mpe-...nisingemruhusu mtu yeyote...Nisingeweza kuigharamia moja, ni ghali mno. Mtu fulani angeninunulia moja, kuna mtu anayeketi papa hapa sasa, angeninunulia moja. Nisingethubutu kumwacha afanye hivyo, huku nikiwa na marafiki wamishenari wasio na viatu, nisingeweza kufanya hivyo, siwezi kuliwazia.

69 Hiyo ndiyo sababu nilijaribu kumpa mtu fulani chapati maji hizi asubuhi ya leo, ninajua njaa ni nini, najua kile hao watu kule wanachopitia. Siwezi kuona vitu vilivyotupwa, wakati mnapojua kwamba ndugu wanaoamini kitu kile kile ninachoamini wako huko wakipitia magumu. Nisingemruhusu kufanya hivyo.

70 Art Wilson alinipa ninii...alimpa Billy Paul muundo 7, au, muundo 70, Roberts .257. Billy, mvulana wangu, anatumia mkono wa kushoto, asingeweza kutumia bolti ya mkono wa kulia. Rafiki yangu anayeendesha Kampuni ya Weatherby alisema, "Vema, hebu nitume hiyo kwa Weatherby naye aitoboe tena, akutengenezee Weatherby kutokana nayo." Kasema, "Haingeninii..." Kasema, "Ingekugharimu kama dola thelathini, inigharimu kama kumi." Akafanya hivyo.

71 Hakuitoboa vizuri, risasi ya kwanza ililipukia usoni mwangu mwote, karibu iniue, na...?...yapata majuma sita yaliyopita, ninii tu...Unaona mahali pale *kule*? Ikagonga jino *hilo* na kuling'oa, ambapo ilipitia *pale*, kisha ikakata sehemu ya uso wangu. Tatu za hizo zikaenda karibu na *pale*, zikishikamana na tezi za pua, na kwenye mfupa. Nazo kumi na tano zikaingia moja kwa moja nyuma ya darubini namna *hiyo*, karibu iipasue hiyo darubini vipande viwili. Inaonyesha tu...

72 Nilipata ujumbe kutoka kwake, uongofu huu wa "kupeana mkono," hivyo ndivyo ilivyokuwa. Mnaona, kama bunduki hiyo ingeanzia mtamboni kama Weatherby Magnum, ingestahimili huo uzito. Lakini kwa kuwa ilichezewa na kujaribu kutobolewa tena...Bila shaka, mtu yeyote mtumia bunduki anajua kilichotokea, ilikuwa na shinikizo upande *huu*. Mnaona? Ikailipua.

73 Hivyo ndivyo ilivyo na baadhi ya hizi dini za "kupeana mikono." Ninaamini katika kuzaliwa mara ya pili, kurudi mwanzoni, na kufa, na kufinyangwa upya. Mnaona? Usipofanya hivyo, kutakuwa na mlipuko mahali fulani safarini, itakulipukia shinikizo linatakapokuja. Basi hebu tudhibiti shinikizo.

74 Nilikuwa huko chini Kentucky pamoja na rafiki yangu, tukiuza vitabu hapa mikutanoni, Bw. Wood. Yeye ni Shahidi wa Yehova ambaye aliongolewa na huyo mvulana mwenye polio aliye naye, ameoa sasa, mguu ukiwa umekunjamana chini yake, labda tutapata nafasi ya kumfanya atoe ushuhuda. Aliokoka, akajazwa na Roho Mtakatifu.

75 Ndugu zake walikuja, baba yake alikuwa msomaji, wakamtenga na watu wao wote. Siku moja ndugu yake aliingia, nikiwa nyumbani likizoni, au, nikipumzika, akashuka kwa nduguye, akasema, "Banks, ati nini" huyo ndiye aliye hapa, kasema, "kwani umejichanganya na nini hasa?" Akasema, "Kundi la ulokole!"

Akasema, "Huo, sio ulokole," akasema, "hebu uuangalie mguu wa David."

76 Akasema, "Aa, upuuzi." Kasema, "Baba yako amekulea, alitulea sisi tangu utotoni tusije tukawaamini wahubiri wa kuzimu inayowaka moto," na kadhalika namna hiyo. Kasema, "Hupaswi kufanya jambo kama hilo." Kasema, "Kwani unamsikiliza tapeli wa namna gani?"

Kasema, "Huyo hapo, huko nje shambani, akilundika nyasi kavu." Karibu na kwao.

77 Akanialika ndani, nadhani nilionekana kama kila kitu ila mhudumu. Naye akasema, akiwa ameketi pale, akasema... Nilikuwa nikizungumza naye. Kasema, "U hali gani?" Baridi sana, asiyejali.

78 Kwa hiyo ono likaja, nikizungumza tu, limetokea papa hapa, mara tatu ama nne tangu nimesimama hapa, mnaona, ndipo nikasema, "Wewe ni...Kwa nini kumwacha mke wako, hao wavulana wawili wadogo?"

Akamwangalia Banks, kana kwamba ndugu yake alikuwa ameniambia hilo.

79 Nikasema, "Usimtazame," nikasema, "hakuniambia hilo." Nikasema, "Vipi kuhusu usiku kabla ya jana? Mke wako ni mwanamke mwenye nywele za kimanjano, ulikuwa na mwanamke aliyekuwa na nywele za kahawia. Huku mtu huyo anabisha mlangoni, nawe ukapitia dirishani. Ni jambo zuri hukwenda, la sivyo kichwa chako kingelipuliwa, mtu alikuwa na bastola mkononi mwake."

80 Akaangukia sakafuni, akautoa moyo wake kwa Kristo, akaokoka. Sasa, familia yake yote imeokoka kwa njia ile ile, kila mmoja wao. Mnaona? Tulikuwa...Wakajazwa na Roho Mtakatifu.

81 Kisha chini...Tulikuwa tukiwinda huko chini Kentucky, na tulikuwa tukiwinda kuchakulo, ninapenda kuwinda kuchakulo, mchezo tu wa kuwinda kuchakulo. Tunapenda kuwala. Niliilenga bunduki yangu kupiga jicho kwa umbali

wa yadi hamsini, mnaona, kwenye—kwenye—kwenye yadi hamsini tu. Kwa hivyo tulikuwa na...Kuwinda, ilikuwa ninii sana...Kama uliwahi kuwinda kuchakulo wa kijivu, umewinda, nadhani, Oklahoma huko juu, wao ni...unanena kuhusu Houdini kuwa bingwa wa kutoroka, yeye sio bingwa wa kutoroka kwa vyovyote vile, ukimlinganisha na mmoja wao. Jinsi wanavyoweza kutoroka mbio namna *hiyo*! [Ndugu Branham alidata vidole vyake—Mh.]

82 Kwa hiyo kulikuwa kukavu sana, usingeweza kuwakaribia, kwa hivyo akasema, "Kuna mahali fulani chini hapa nda—ndani, mzee ambaye tungeweza kuwinda huko chini mabondeni ambako kuna unyevunyevu." Unajua *uwazi* ni nini? Tunaloita *uwazi*, ni bonde ambapo vilima vinashuka, basi unapitia mahali hapa, unaangalia pande zote mbili za kilima, kuna unyevunyevu ambapo maji hutiririkia.

83 Akasema, "Ila yeye ni kafiri, na mmojawapo wa watu wakali sana nchini." Kisha akasema, "Loo, yeye ni mbaya sana." Kasema, "Anajua, wewe ukiwa mhubiri," kasema, "yeye... Hmm!"

Nikasema, "Vema, hebu twende tujaribu."

84 Kwa hiyo tukashuka kupitia migongo ya hivyo vilima, na kuingia mabondeni, na kila kitu, mpaka tukarudi, mbali sana kondeni. Hapo palikuwa na maskini nyumba nzuri huko nyuma, jamaa mzee mwenye kofia kubwa ya kuelemea chini, wawili wameketi pale, mwajua, chini ya mti. Akasema, "Yule pale."

Kwa hiyo nikasema, "Wewe ongea." Kwa hiyo tukakaribia kwa gari, naye akatoka nje, akazungumza naye.

Kasema, "Karibu ndani." Mnajua jinsi Wakentaki, wakusini...Kasema, "Karibu ndani."

85 Akaketi pale kidogo, na kusema, "Jina langu ni Wood," kasema, "Mimi ni Banks Wood." Kasema, "Sijui kama tungeweza kuwinda," kasema, "rafiki yangu yuko hapa chini." Kasema, "Tumekuwa tukiwinda hapa kwenye kile kijito kingine," kisha kasema, "ni kukavu sana, tulifikiri labda..."

Akasema, "Wewe ni Wood yupi? Je, wewe ni mvulana wa Jim Wood?"

Kasema, "Naam."

Akasema, "Jim Wood ni mtu mwaminifu katika nchi hii," kasema, "yeyote wake au wa watu wake, nina mamia ya ekari hapa, karibu."

Kasema, "Asante, bwana." Kasema, "Je, ni sawa kwa mchungaji wangu," hakukusudia kusema hivyo, mnaona, "mchungaji wangu akienda nami?"

Akasema, "Usiniambie ya kwamba wa Wood amekuwa duni sana inambidi kubebana na mhubiri popote aendapo?"

Kasema, “Naam.” Kasema . . .

Nikawazia wakati wa mimi kutoka nje ulikuwa umewadia. Kwa hivyo nikashuka kwenye hilo gari, nikazunguka, nikasema, “Mu hali gani?”

Naye akasema, “Nawe ni mhubiri ati?”

86 Sikuwa nimeoga kwa najuma mawili, mwajua, na damu ya kuchakulo, na masharubu marefu *hivyo*. Nikasema, “Naam, bwana.” Nikasema, “Nakisia sionekani kama mmoja.”

Akasema, “Vema, sehemu hiyo ni sawa, lakini,” kasema, “unajua, ninadhaniwa kuwa ni kafiri.”

Nikasema, “Hilo si jambo la kujivunia sana, sivyo, bwana?”

Akasema—akasema, “Sidhani.” Akasema, “Lakini kitu pekee nina—ninachowazia ni . . . ”

Nikawazia, “Bwana, kama uliwahi kunisaidia, fanya hivyo sasa, maana ni—nina . . . jambo fulani halina budi kutukia.”

87 Akasema, “Vema, jambo pekee nililo nalo dhidi yenu ninyi jamaa, mnabwekea tu mti usiohusika.” Yupo mtu anayejua maana ya huo? Mbwa mwongo, mwajua, yule anayebwekea mti *huu*, wakati kuuni yuko kwenye mti mwingine, mwajua. Hivyo akasema, “Mnabwekea mti usiohusika,” kasema, “unaongea kuhusu kitu fulani, huku hakuna kitu kabisa huko juu.”

Nikasema, “Vema, labda hilo ni kwa maoni.” Mnaona? Nikasema, “Labda huyo mbwa huona kitu ambacho hukioni.” Hmm?

Naye akasema, “Vema,” kasema, “kwanza kabisa hakuna kitu huko juu.” Kasema, “Hakuna kitu kama Mungu.”

Nikasema, “Vema, hayo ni majaliwa yako ya Marekani kuamini hivyo.”

88 Na kwa hiyo, kulikuwa na mti wa tofaa wa kale umesimama pale, na—na mengi yao huanguka chini, mwajua. Ilikuwa karibu katikati ya Agosti, nao manyigu walikuwa . . . Mnajua nyigu ni nini? Walikuwa wakiyanyonya hayo matofaa moja kwa moja, mwajua. Kwa hiyo nikasema . . . niliwazia afadhali nibadilishe hiyo mada haraka sana, mwajua, kwa hivyo nikasema, “Unajali kama nikila mojawapo ya matofaa hayo?”

89 Akasema, “Loo, hata kidogo.” Kasema, “Manyigu wanayala.” Kwa hiyo nikainama na kuokota moja, nikalisugua tu kwenye ovaroli chafu. Unapokuwa Rumi, huna budi kuwa Mrumi, mnajua.

Kwa hiyo nikasema, “Vema . . . ” Nikaliuma hilo tofaa, na kusimama hapo kidogo.

90 Akasema, “Naam, hiyo ndiyo shida yenu enyi jamani, nyinyi sikuzote,” kasema, “jambo pekee ni kwamba, mnawakamua watu, mkiishi kwa msaada.”

91 Nikasema, "Naam, hiyo ni kweli, tunaishi kwa sadaka za watu, za hiari. Si lazima waje. Unaona? Wanaiamini, nao wanaiunga mkono."

92 Akasema, "Vema," akasema, "hakuna kitu kama hicho. Sijawahi kuona chochote kikitangaza mambo kama hayo." Kasema, "Ninaweza kutazama juu sana kadiri ya upeo wa macho yangu, simwoni Mungu, sioni kitu kingine chochote." Kipofu sana, mwajua. Na hivyo, akasema, "Sioni chochote, sioni Mungu. Nimekuwa hapa kwa miaka sabini na sita, wala sijaona chochote bado."

93 Akasema, "Nitasema jambo moja, kulikuwa na mhubiri mmoja, wakati mmoja, yapata miaka miwili iliyopita, aliyekuja hapa Acton, kwenye uwanja wa kambi ya Methodisti." Kasema, "Alikuwa ni jamaa kutoka huko *Indiana'r*." Akasema, yeye . . . "Bi Kizee Casshorn," naamini ndilo lilikuwa jina lake, kasema, "anaishi hapa juu ya kilima, moja kwa moja huko juu." Kisha kasema, "Alikuwa na kansa tumboni." Kisha kasema, "Mimi na mke wangu tulikuwa tukipanda huko kila asubuhi," kasema, "hatungeweza kumweka kwenye maliwato ya kitandani tena," samahani hili akina dada, lakini ninyi nyote . . . ? . . . mnaona, lakini kasema, "tulilazimika tu kutumia shuka la kuvuta," mpira chini, mwajua, "na kuvuta hilo shuka." Kasema, "Mimi na mke wangu tulikwenda huko kila asubuhi na kila jioni, na kubadilisha kitanda chake na kumwandaa. Yeye na mumewe wanaishi huko juu." Kisha kasema, "Madaktari walikuwa wakimwona," na kusema, "alikuwa akitibu kansa hii kwa takriban mwaka mmoja." Kisha kasema, "Alikuwa amefikia mahali ambapo hata hawakurudi tena, akiishi tu kwa dawa za kulevya."

94 Kasema, "Mhubiri huyu alikuwa anatoka *Indiana'r*, hakuwahi kuja humu ndani hapo kabla," kisha kasema, "nao, wakiwa na mkutano kule juu." Kasema, "Ilikuwa, nadhani kulikuwa na yapata watu elfu moja na mia tano kwenye huu . . . " Acton ni mdogo, mdogo sana . . . Vema, nadhani idadi ya watu ni kama ishirini, mnaona, lakini wana uwanja wa kambi huko.

95 Na kwa hiyo, akasema, "Usiku wa pili pale alipokuwa akihubiri," kasema, "aliliangalia hilo kusanyiko, kisha akamwambia dada yake mwanamke huyu, akamwita kwa jina, na kumwambia alipotoka nyumbani alichukua leso ndogo nyeupe yenye mchoro mdogo wa bluu pembeni mwake, naye alikuwa ameiweka kwenye kibeti chake cha mfukoni; alikuwa na dada mmoja jina lake *Nanii* hapa aliyekuwa yuafa kwa kansa, njoo, uweke leso hii juu yake, naye atapona."

96 Kisha kasema, "Usiku huo yapata saa nne," kasema, "Nilifikiri walikuwa na Jeshi la Wokovu kule juu ya kilima,

sijawahi kusikia kelele nyingi hivi maishani mwangu. Tulidhani huyo bi kizee alikuwa amekufa."

97 Kwa hiyo, Kentucky, wanalala saa moja pamoja na kuku, mwajua, wanaponinii. . . Hivyo basi. . . Hivyo wakasema. . . Na huyo alikuwa Big Ben, mwajua, ambaye alipeleka leso hiyo, na akapanda kule pamoja na mama huyo kumwekelea (Naye anaweza kulia vikali kama chui mweusi, kwa vyovyote vile, mwajua.), huko juu kilimani. Kwa hiyo, alikuwa huko juu.

98 Naye akasema, "Kesho yake asubuhi tulipanda tujue kile tungeweza kuwasaidia nacho." Bila shaka huko nyuma, usingeweza kupata mzishi hadi asubuhi, mwajua. Kasema, "Tukapanda—tukapanda huko juu, tuone kile tungeweza kufanya, mimi na mke wangu." Kisha kasema, "Tulipofika kule juu," kasema, "mwanamke huyo alikuwa akila sambusa za matofaa yaliyokaangwa, ameketi mezani, akinywa kikombe cha kahawa, yeye na mumewe."

99 Mnajua sambusa za matofaa yaliyokaangwa ni nini, nusu-mwezi? Mnaona, unakanda unga kama chapati maji, na kuweka ninii. . . Mnajua ni nini—mnajua maharagwe ya maganda, maana ya maharagwe ya maganda? Mnaona, maharagwe unayoyaweka, unajua, unayaanika yakaushwe na jua, kisha unayakausha matofaa, unajua, vivyo hivyo, juu ya nyumba. Kisha unachukua matofaa haya na kuyaweka humu ndani, unayageuza namna *hiyo*, kisha unayakaanga, kufanya kile wanachokiita "nusu-mwezi," unatia molasi ya mtama juu yake, ni tamu sana. Na. . . [Ndugu mmoja anasema, "Ni nzuri."—Mh.] Ni nzuri, hakika ni nzuri. Na kwa hiyo. . .

100 Kasema, "Alikuwa akila sambusa za matofaa yaliyokaangwa, yeye na mumewe." Kisha kasema, "Hafanyi tu kazi yake mwenyewe, bali anafanya kazi ya jirani tangu wakati huo. Kwa hiyo sasa, nilitaka kujua jinsi mtu huyo alivyojua jambo hilo."

Naye Banks alikuwa akinitazama. Akaanza-. . . Nikamtikisia kichwa *hivyo*.

Naye akasema, "Ningependa kujua. . . "

Nikasema, "Humaanishi hiyo ni kweli." Nikasema, "Usingeweza kuamini kitu kama hicho."

101 "Vema," kasema, "Ninaweza kukupandisha kule juu na kukuthibitishia hilo." Mnaona, sasa alikuwa akinihubiria wakati huo, mnaona, nikamwacha. . . Akasema, "Ninaweza kukupeleka huko juu na kukuthibitishia hilo."

Nikasema, "Loo, ninaamini usemalo." Mnaona? Nikasema, "Ninaamini usemalo."

102 Akasema, "Vema, yeye yuko pale pale. Na kama huamini, panda tu kule ukaulize, na umwulize jirani yeyote hapa, yeyote kati yao anaweza kukwambia kuhusu hilo."

“Loo,” nikasema, “Mimi . . . u—unamaanisha hiyo ni kweli?”

Akasema, “Hakika ni kweli.”

103 Nami nikawazia, “Uh-huh. Sasa, unanihubiria tena.” Mnaona? Nikasimama pale kidogo tu, ndipo nikasema . . . Akasema . . . Nikasema, “Vema, ni nini . . . U—ulitaka kumwona huyo mhubiri kuhusu nini? Jina lake lilikuwa nani?”

Kasema, “Sijui.” Kasema, “Kama nitawahi kumwona, nitamwuliza kuhusu hilo.”

Nikasema, “Naam, bwana. Vema,” Nikasema, “Natumaini utamwona.”

104 Naye akasema, “Vema,” akasema, “unajua,” akasema, “jambo nisiloweza kuelewa ni yale ali—alikuwa anazungumzia wakati angeweza kusimama pale, wala hajawahi kuwa katika nchi hii hapo kabla, na kujua kwamba mwanamke huyo ana leso hiyo, na kutumwa kule, na kuiweka juu ya mwanamke huyo, na kumwambia hasa yale yatakayotukia. Hiyo imekuwa miaka miwili iliyopita, naye ni mzima kabisa,” kasema, “na yeye—yeye ni mzima.”

105 Kasema, “Huyo hapo, madaktari walisema angekufa dakika yoyote, walimpasua akiwa na kansa, kisha wakamshona tu, wasingeweza kufanya lolote juu yake, ilikuwa imeenea,” mnaona, kasema, na kwa hiyo, akasema, “wakamfunga.” Kisha kasema, “Huyo hapo.”

Nikasema, “Vema, hiyo hakika inashangaza, sivyo?”

Naye akasema, “Hakika inashangaza.”

Nikasema, “Jamani, hilo ni tofaa tamu.”

Naye akasema, “Naam, hilo ni tamu.” Kasema, “Hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Mti huo una umri gani?”

106 Akasema, “Ewe kijana,” miaka yangu yote hamsini, mwajua. Akasema, “Ewe kijana,” akasema, “Nilikuwa nikiishi kule juu ya kilima kile. Mimi, na babangu, na mamangu, nasi sote tuliishi kule juu, palipo na ile me—meko ya kale, ile nyumba ya kale ya magogo.” Kasema, “Baba akajenga nyumba hii, nasi tukahamia huku chini,” kasema, “alipokufa, nikairithi,” kasema, “nimeilelea familia yangu hapa.” Kasema, “Mimi nina sabini na sita.”

107 Akasema, “Niliupanda mti huo, hapo, yapata miaka arobaini na mitano iliyopita.” Kisha kasema, “Umetoa zao zuri la matofaa kwa ajili yangu tangu ulipoanza kuzaa.”

Nikasema, “Ajabu.” Nikasema hiyo ni . . . ? . . . Nikasema, “Ninaona majani yote yanaanguka kutoka kwenye mti huo.”

108 Angalieni, mama yangu mkongwe alizoea kuniambia, “Mpe tu ng’ombe kamba ya kutosha, atajinyonga.” Mnaona? Kwa hiyo mfunge tu farasi wako nchani mwa kamba, mwangalie

wakati akiweka mguu wake juu yake baada ya kitambo kidogo, unajua. Basi hivyo ndivyo, bila ninii yoyote. . .Inanibidi tu kumtegemea Mungu, urahisi tu wa kusikiliza, nawe ukienda tu jinsi Yeye anavyoongoza, unaona. Pasipo—pasipo na nguvu za akili zangu mwenyewe kuwakatilia mbali hao jamaa werevu, mwajua, inakubidi tu kumwacha Yeye afanye hivyo, unaona.

Kwa hiyo akasema, "Vema," akasema, "naam, majani yanapukutika."

109 Nikasema, "Sasa, hilo ni jambo la kushangaza, sivyo, bwana?" Nikasema, "Haya basi. . .Hii hapa katikati ya Agosti, tuna. . . " Bado kulikuwa na joto, takriban tisini papo hapo kivulini. Nami nikasema, "Katikati ya Agosti bila jalidi yoyote wala kitu chochote, na bado hayo majani yanapukutika kutoka mtini." Nikasema, "Nashangaa ni nini kinachosababisha hilo."

"Loo," akasema, "u—uhai uliyaacha."

"Loo," nikasema, "Kumbe, uhai uliyaacha. Kwani huo uhai ulienda wapi?"

Akasema, "Chini ya mizizi, utomvu."

"Loo," nikasema, "kumbe?" Naye akasema. . .Nami nikasema, "Kwa nini unafanya hivyo?" Nikasema, "Unataka kusema kwamba uhai huo hauko huko juu ya mti huo kwenye majira ya baridi kali?"

Kasema, "La, la. Ingeuua, chembe ya uhai ingeuawa humo mtini kama ukibaki huko juu." Kasema, "Uhai hushuka moja kwa moja hadi kwenye mizizi."

"Uh-huh," nikasema, "unarudi kwenye majira yajayo ya kuchipua, unakuletea lundo lingine la matofaa."

"Naam."

110 Nikasema, "Nataka unijibu swali." Nikasema, "Niambie, mti huo hauna akili yoyote, lakini kuna Akili maalum sana inayouambia mti huo kwamba 'Sasa, inakuja, ni majira ya baridi kali, toka hapo, urudi chini kwenye mizizi na kujificha, chini ya udongo, majira yajayo ya kuchipua huna budi kumletea jamaa huyu matofaa.' Na usipomjali Huyo, unakufa. Kama kweli ukimjali, unaendelea kuishi, hiyo Akili, hauna budi kuijali Akili hii."

Akasema, "Vema, hayo ni maumbile tu."

111 Nikasema, "Maumbile ni kitu gani?" Nikasema, "Unamaanisha kijiografia tu, na kutikisika kwa ardhi?" Nikasema, "Hebu weka ndoo ya maji huko nje kwenye ile nguzo katikati ya Agosti, acha tuone ikishuka hadi chini ya nguzo, halafu katika majira ya kuchipua yarudi juu, na kuwa na ndoo nyingine ya maji."

Kasema, "Hayatafanya hivyo."

Nikasema, "Vema, basi, lazima iwe ni Akili fulani inayoudhibiti huu." Mnaona?

Kasema, "Sikuwahi kamwe kuliwazia jinsi hiyo, lakini nadhani umesema kweli."

112 Nami ni—nikasema, "Vema, basi, utakapogundua ni Akili gani inayouambia utomvu huo—huo hivyo kwenye mti huo kushuka chini kwenye mzizi ukajifiche, urudi tena, na kuleta kitu fulani cha kumfaidi mtu fulani, nitakwambia Akili iyo hiyo ndiyo iliyoniambia kwamba mwanamke huyo alikuwa amelala pale akifa kwa kansa, na kama angetii amri za Mungu, angeponywa."

Akasema, "Kweli wewe siye mhubiri yule?"

Nikasema, "Ndimi."

"Jina lako ni nani?"

Nikasema, "Branham."

Akasema, "Huyo ndiye yule jamaa. Je, unaweza kulithibitisha?"

Nikasema, "Vema, nadhani ningeweza." Na hapo chini ya mtofaa huo, pamoja na kitu hicho kidogo rahisi, *Uhai*, nikamwongoza kwa Kristo.

113 Mwaka jana nilikuwa huko chini tena, nikaenda kwenye huo mti, naye mwanamke mmoja alikuwa ameketi nyuma pale, mkewe, akimenya matofaa. Nikamwulizia, alikuwa ameaga dunia.

114 Akasema, "Bw. Branham, Mungu awe pamoja nawe daima." Akasema, "Mwaka baada ya mwaka tulijaribu, tulifanya kila kitu, lakini hadithi hiyo ndogo rahisi kuhusu mtofaa, ilimleta kwa Kristo."

115 Kwa hivyo uzima ni rahisi sana, lakini hata hivyo, ni mkuu sana. Hebu tuweke tu kile tulicho nacho, ili tuwe na ufufuo siku moja, wala sio sisi tu, hebu tumlete mtu mwingine pamoja nasi tutakapofikia siku hiyo. Hiyo ni sawa? Je, twaweza kuomba?

116 Baba wa Mbinguni, uliufanya uzima kuwa rahisi sana, njia rahisi sana, dhahiri sana. Na iwe mbali nasi kujaribu kamwe kuipotosha hi—hivi kwamba tuyaingize yetu, yale tunayowazia, akili. Hebu tuchukue tu urahisi ambao Mungu ameuweka mbele zetu pale, tuutumie huo kuwaleta watu kwa Kristo.

117 Baba Mungu, tuko hapa sasa, tuko hapa kufungua mkutano huu. Kuna wenye dhambi huku kote, sijui wao ni akina nani, mahali walipo. Mimi huyu hapa nimeketi na wanaume na wanawake, asubuhi ya leo, ninaoamini kwamba kote katika nyakati zijazo zisizo na mwisho kwamba tutaishi pamoja. Tunapoketi hapa, asubuhi ya leo, tukitazamana mezani, ninaangalia kupitia mstarini, nikiwaona watu wenye mvi ambao pengine walikuwa hudumani, wakihubiri, nilipokuwa mwenye

dhambi, tulipeana mikono, tukashirikiana kwenye kifungua kinywa chetu.

118 Huenda tusikutane tena kwenye kifungua kinywa kingine, lakini kuna jambo moja hakika, tutakutana kwenye Karamu siku moja, hiyo ni Karamu ya Arusi, wakati meza hiyo kuu imetandazwa kote angani, kutoka anga hadi anga. Tutaangaliana mezani, hapana shaka kutakuwako na tone la chozi dogo kutoka mashavuni mwetu, tunapowazia, tunapopeana mkono, tuseme, "Nakumbuka ule mkutano wa Salem. Huyu hapa Ndugu *Nanii*, yeye ndiye aliyeingia wakati huo; huyu hapa chini."

119 Ndipo Mfalme katika uzuri Wake atatokea amevikwa mavazi Yake meupe, afute machozi yote kutoka kwa macho yetu, aseme, "Msilie, enyi watoto, yote yamekwisha. Ingieni katika furaha za Bwana zilizoandaliwa kwa ajili yenu tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu."

120 Mungu, jalia tuwe na wengi wanaoketi mezani kwa sababu ya juhudi hii tunayofanya. Sasa, tutafanya yote tuwezayo, Bwana, tunakutegemea Wewe utusaidie. Sisi ni Wako, tuko mikononi Mwako, Bwana, fanya nasi upendavyo.

121 Tunakushukuru kwa ushirika wa sisi kwa sisi, na pamoja na Mwana wa Mungu, ambaye Uwepo Wake uko pamoja nasi sasa. Na adumu milele, na jalia tudumu waaminifu na wakweli kwa wito, ili tuweze kutoka, si katika uwezo wa fedha, katika uwezo wa mambo makuu ya dunia, lakini kwa nguvu za unyenyekevu, katika utamu na unyenyekevu wa Roho, kama Yeye atakavyotufanya na kutufinyanga kuwa mifano ya wana na binti za Mungu, ili tuweze kuwaleta wengine Kwake. Katika Jina la Yesu, tunaomba baraka hii tupate kumheshimu Mungu. Amina.

122 Asanteni sana, marafiki. Mkipenda, nitaninii, ni—nitalipia kifungua kinywa chenu. Nilikuwa na wakati huu wa ushirika, nitafurahia kufanya hivyo. [Ndugu mmoja anasema, "Hatupendi kuwa wakaidi, hatupendi, fanya hivyo, ingawaje."—Mh.] Naam, ni—nitafurahia kufanya hivyo. Mnaona? Ni—nitafurahia kuifanya. Bila shaka nimefurahia kuwa hapa na kuwa pamoja nanyi. Na sasa, mpaka nitakapowaona usiku wa leo, ndugu yetu, mwenyekiti, njoo.

62-0719B Uzima
Marion Hotel
Salem, Oregon Marekani

SWAHILI

©2024 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

Voice Of God Recordings
P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.
www.branham.org